# TAMKO:

Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ni mji ambao umezungukwa na vilima ambavyo vimeufanya mji kuwa na mandhari nzuri na ya kuvutia. Ardhi ni nzuri kubwa na ya kutosha kwa shughuli zote za uwekezaji.

Barabara zimetengenezwa kwa viwango vinavyofanya barabara kupitika kwa vipindi vyote vya majira ya mwaka. Zipo huduma za mawasiliano kama vile usafiri wa reli na anga (ndege), upatikanaji wa uhakika wa maji na umeme unaokidhi uhitaji wa wakazi wa Manispaa na hata kwa watakao hitaji kuwekeza.

Manispaa ya Dodoma imekuwa ikipanuka kwa kasi kutokana na ongezeko kubwa la wahamiaji, ujenzi wa makazi, vyuo na vyuo vikuu vimeufanya mji huu kuwa kitovu cha elimu, pia biashara imepanuka na kuongeza pato la mwananchi wa kawaida.

Maeneo makuu yauwekezaji yaliyowazi ni maeneo ya kilimo, ujenzi na uendelezaji wa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali, elimu na ujenzi wa makazi. Jarida hili limeainisha vipaumbele kwa wawekezaji wa ndani na wa nje wanaotaka kuwekeza katika Halmashauri yetu ya Manispaa.

Mwelekeo wa Halmashauri ya Manispaa, ni kuendelea kuboresha na kutoa huduma endelevu za kijamii

na uchumi, kuimarisha amani na utulivu, kulinda na kuhifadhi mazingira, kuwezesha jamii kusimamia maendeleo yao wenyewe na kupiga vita umaskini.

Dira ya Manispaa ya Dodoma katika kipindi cha miaka kumi ijayo, inadhamiria kuboresha huduma za kiuchumi, na kijamii, kuimarisha utawala bora, kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu. Haya yote yanawahakikishia wawekezaji.hali ya ulinzi na usalama.

Jarida hili limeandaliwa kwa kushirikiana na ofisi ya Mchumi wa Manispaa, Duwasa, Tanesco, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mamlaka ya viwanja vya Ndege Dodoma, CETAWICO, Shirika la Reli - Dodoma, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana Dodoma, Mzee Ernest Kongola, Ndugu Willy Mwangason na watu wengine ambao hawajatajwa hapa lakini wameshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa ushiriki wao ambao umepelekea kufanikisha kazi hii.



**Suzan E. Bidya**

*Mkurugenzi Manispaa Dodoma*

**Yaliyomo:**


- **Neno toka kwa Mkurugenzi 1**
- **Utangulizi 2**
- **Historia ya Dodoma 3**
- **Ongezeko la watu 4**
- **Mahali ilipo 4**
- **Hali ya hewa 5**
- **Ardhi na matumizi yake 5**
- **Utawala 6**
- **Elimu 6**
- **Afya 6**
- **Miundo mbinu 6**
- **Reli 7**
- **Uwanja wa ndege 7**
- **Mawasiliano 8**
- **Huduma za kifedha 8**
- **Huduma ya umeme 8**
- **Maji safi na maji taka 8**
- **Uchumi katika manispaa 9**
- **Uwekezaji katika kilimo 9-11**
- **Uwekezaji katika viwanda 9-11**
- **Machinjio ya Dodoma 12**

# HALMASHAURI YA MANISPAA DODOMA

## UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ni moja wapo kati ya Halmashuri sita (6) katika Mkoa wa Dodoma. Halmashauri nyingine ni Chamwino, Bahi, Kongwa, Mpwapwa na Kondoa. Manispaa ya Dodoma ina ardhi nzuri na yakutosha, upatikanaji wa uhakika wa Maji na umeme, barabara, reli, uwanja wa ndege na mazingira mazuri kwausalama wa wawekezaji wote wa ndani na wa nje. Halmashauri imepitiwa na barabara kuu ya kaskazini itokayo Afrika kusini hadi Cairo Misri. Pia ni makutano ya barabara kuu nne (4) ambazo ni kutoka mashariki kwenda magharibi yaani Dar es Salaam-Kigoma/Rwanda, Burundi. Kaskazini kwenda kusini yaani Arusha-Mbeya/Tunduma aidha Manispaa yetu imepitiwa na Reli ya kati itokayo Dar es Salaam-Tabora, Mwanza/Kigoma.

## HISTORIA YA DODOMA

Miaka mingi iliyopita mji huu ambao leo unaitwa Dodoma ulikuwa ukifahamika kama Calangu (Chalangu) mji huu haukuwa na wenyeji bali walikuwa wahamiaji toka maeneo mengine ambayo ni wamanghala, wabambali, wayenzele na wanghulimba. Wahamiaji hawa walikuwa wakitofautiana kwa tabia zao, wamanghala na wabambali waliishi msituni na walikuwa wawindaji wakila nyama na asali. Na wayenzele na wa wanghulimba walikuwa wakulima na wafugaji. Watu hawa walikuwa waoga kiasili hivyo watu wengine walipoanza kuingia kutoka maeneo ya kaskazini

wambugwe, magharibi wanyamwezi na kusini wa hehe watu hawa waliondoka na kwenda kuishi sehemu nyingine.

Sababu ya wahamiaji hawa kuitwa wagogo, neno hili linatokana na wafanyabiashara wakinyamwezi walipokuwa wakipita na bidhaaa zao kuelekea Pwani kwa biashara, walipofika kati ya Itigi na Manyoni walikuta mti mkubwa umeanguka na kuzuia njia, hivyo kwa muda mrefu wali lazimika kulala upande mmoja kabla ya kuvukia upande wa pili wa mti (gogo). Hali hii iliwafanya kila walipo ulizwa wanalala wapi kabla ya kuendelea na safari walisema wanalala kwenye limgogo. Kwa hiyo wahamiaji hawa wakafahamika kama gogo (wagogo) kutokana na gogo hilo.

Mnamo mwaka 1912 alifika mjerumani Dr. Spreling (Spelenje), na kuanzisha ngome yake, ngome hiyo kwa sasa ni ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi aliyokuwa akifanyia kazi za utawala na utoaji maamuzi kwa wahalifu (kufungwa, kuchapwa viboko na kunyongwa) kwa sasa ni Ofisi ya CCM Wilaya ya Dodoma Mjini. Bustani aliyopenda kutembelea na kupumzika ilikuwa eneo la Kikuyu ambayo kwa sasa ni Chuo Kikuu cha St. John's, eneo hili kwa wakati huo lilikuwa tepetepe na mapitio ya wanyama wakitokea mbuga za kaskazini (Arusha) kuelekea mbuga za kusini (Mikumi). Mapitio ya wanyama hao ndio yaliyo sababisha kubadilika kwa jina la eneo hili baada ya tembo kudidimia katika eneo hilo tepetepe karibu na shule ya sekondari mazengo ambayo sasa ni chuo kikuu cha ST.JOHNS. Kitendo hiki cha kudidimia kwa lugha ya Kigogo inajulikana kama IDODOMIA hivyo baada ya kitendo hiki jina likabadilika kutoka Calangu (Chalangu) nakuwa Idodomia (DODOMA).

*Jengo lililokuwa ngome ya Dk. Sperling*

*Jengo la iliyokuwa ofisi ya utawala*

*Mti uliotumiwa kunyongea wahalifu*



*Eneo alilozama tembo*

Mji wa Dodoma ulitangazwa rasmi kuwa makao makuu ya Chama na Serikali chini ya kifungu cha sheria No.320 ya mwaka 1973. Baada ya hapo matukio ya mafanikio yalifuata. Mwaka 1980 mji wa Dodoma ulipewa hadhi ya kuwa Manispaa. Mwaka 1995 serikali iliamua kuwa shughuli zote za bunge zifanyikie Dodoma. Bunge lilianza shughuli zake rasmi mwezi Februari 1996.




*Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.*

## ONGEZEKO LA WATU

Halmashauri ya Manispaa ina jumla ya wakazi (watu) 462,968 wakiwemo wamaume 227,978 na wanawake 234,990 wastani wa ongezeko la watu kwa 4.0% ukilinganisha na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 ambayo jumla ya watu ilikuwa 324,347 wakiwemo wanaume 157,469 (48.5%) na wanawake 166,878 (51.5%).

## MAHALI ILIPO


Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ina ukubwa wa kilometa za mraba 2769 ipo latitudo 6.00˚ na 6.30˚ kusini longitudo 35.30˚na 36.02˚ mashariki. Mwinuko kati ya mita 600-1000 juu ya usawa wa bahari. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 196,000, eneo la malisho ni hekta 44,028 na eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 3,000. Halmashuri ya Manispaa inezungukwa na wilaya ya Chamwino kwa upande wa mashariki na wilaya ya Bahi kwa upande wa magharibi.

## HALI YA HEWA

Hali ya hewa ya Dodoma ni ya kati/wastani (nusu jangwa) imegawanyika kwa majira mawili (2), ma jira ya mvua (masika) na majira ya ukame wa muda mrefu (kiangazi). Majira ya mvua huanza mwishoni mwa mwezi novemba mpaka mwishoni mwa mwezi aprili. Wastani wa mvua kwa mwaka ni kutoka 550-600mm na wastani wa joto ni kati ya 10˚C mwezi julai hadi 20˚C mwezi Novemba. Mwezi julai ni baridi sana wakati mwezi ni joto kali lisilopungua 30˚C kwa siku.

# ARDHI NA MATUMIZI YAKE

Halmashauri ya manispaa ardhi yake ina rutuba ya wastani yenye udongo unaopitisha maji kiasi eneo linalo tumiwa kwa kilimo ni hekta 145,240. Yakiwemo mazao ya biashara kama zabibu hekta 2257 , ufuta hekta 9924, alizeti hekta 19,992 na karanga hekta 18,463 ambazo huleta jumla ya hekta 50,636. Hekta 94,604 zilizobaki ni kwa mazao ya chakula yaani mtama, uwele, muhogo, mahindi, viazi vitamu, kunde, njugu mawe.




*Ramani ya Mkoa Dodoma*

## UTAWALA

Halmashauri ya manispaa kiitawala ina jumla ya tarafa nne (4), ambazo zinajumla ya kata 37, vijiji 39 na mitaa 88. Kati hizo kata 22 ni za mjini na 15 ni za vijijini.

Upatikanaji wa kazi. Kati halmashauri yetu kuna fursa nyingi za ajira katika Nyanja zote za utaalamu, biashara na kiuchumi. Kipato cha mwananchi wa Dodoma kimeongezeka kwa 41% kutoka 170,000 kwa mwaka 2005 hadi 240,000 kwa mwaka 2009.

## IDARA YA ELIMU.

Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ina jumla ya shule za msingi 107 kati ya hizo shule za serikali za serikali ni 92 na za binafsi ni 15, aidha kuna shule 97 zenye madarasa 85 ya Elimu ya Awali katika shule za serikali na madarasa 12 ya Awali katika shule za binafsi.Na kwa upande wa sekondari kuna jumla ya shule 52 kati ya hizo 36 ni za serikali na 16 ni za binafsi. Katika Halmashauri ya Manispaa kuna vyuo vya Elimu ya juu vipatavyo 6 ambavyo ni CHUO KIKUU CHA DODOMA (UDOM), ST JONS, CHUO CHA MIPANGO, CHUO CHA BIASHARA(CBE) MADINI,na CHUO KIKUU HURIA. Kati ya hivyo 5 ni vya serikali na cha binafsi ni kimoja (1).Pamoja na kuwa na vyuo hivyo vya Elimu ya juu pia tuna CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA-HOMBOLO ni cha serikali na CHUO CHA UALIMU-CAPITAL cha binafsi.

## IDARA YA AFYA

Lengo la Halmashauri ya Manispaa ni kuhakikisha kuwa huduma za Afya zinasogezwa karibu na Wananchi kwa kila kijiji kuwa na Zahanati.Kwa sasa Halmashauri ina jumla ya Zahanati 48, kati ya hizo 6 ni za binafsi.Vituo vya Afya ni 8, vya serikali ni 7 na binafsi ni kimoja(1).Halmashauri ina Hospitali 3 mbili (2) ni za serikali(Hospitali ya Mkoa na Hospitali ya Mirembe) na moja(1) ni ya binafsi DCMC(DODOMA CHRISTIAN MEDICAL CENTER). Halmashauri inajitahidi kudhibiti malaria kwakugawa vyandarua vyenye viatilifu, kutoa dawa za kuzuia malaria kwa wajawazito na kutoa Elimu kwa Wananchi jinsi ya kujikinga na malaria na maambukizi mapya ya UKIMWI.

## MIUNDOMBINU

**Barabara:**

Halmashauri ya manispaa ina barabara nzuri ambazo hutumika vipindi vyote vya mwaka, masika na kiangazi. Zenye jumla ya urefu upatao kilometa 565.1 kati ya hizo km 45.6 ni lami sawa na 8.7%, km 91.8 ni changarawe sawa na 17.0% na km 385.7 barabara ya vumbi sawa 73.7%. Barabara iunganishayo Dodoma-Dar es Salaam ni lami, Dodoma-Singida ni lami ingawa haija kamilika vema. Dodoma-Iringa, Dodoma-Arusha bararbara hizo ni za kokoto iliyoshindiliwa vizuri na pia zipo kwenye mpango wa kuwekwa lami.



*Picha ya barabara mojawapo mjini kati*

Barabara hizo zitakapokamilika kwa kiwango cha lami zitarahisisha usafiri vilevile kufunguka kwa masoko na kupanuka kwa biashara, kwani mkoa wa Dodoma upo katikati ya nchi.

## Reli

Manispaa imepitiwa na reli ya kati itokayo Dar es Salaam-Mwanza/Kigoma. Reli hii hutumiwa na wananchi wa mikoa yote ambayo reli imepita. Kama Morogoro, Singida, Tabora na Shinyanga. Reli hii hutumika kusafirishia mizigo na watu waendao nchi za jirani, ambazo ni Rwanda na Burundi.




*Stesheni ya Dodoma*

## UWANJA WA NDEGE

Mji wa Dodoma una huduma ya usafiri wa anga. Uwanja huu wa ndege wenye ukubwa wa hekta 98 upo eneo la Area C Dodoma na ulijengwa kati ya mwaka ya 1947 na 1948. Aina ya ndege zinazotua katika uwanja huu ni Fokker 50, 28 na Cessna.

Pamojo na kuwa na uwanja huu wa ndege,Serikali ina mpango wa kujenga uwanja mkubwa wa Kimataifa unaotarajiwa kujengwa eneo la kitelela nje kidogo ya mji, utakuwa ni mkubwa na wakisasa wenye huduma zote muhimu ambazo hupaswa kuwepo kwenye viwanja vikubwa vya ndege.Utakuwa na ukubwa wa mita za mraba

4,515,342.00 (9km x 4.5km), aina za ndege zinazotarajiwa kutua katika
Uwanja huo ni ndege aina ya Boeing 737 Family (B.737-100, B.737-200…….) pia ndege aina ya
B.737-900, 900ER. Uwanja huu utakapo kamilika utawapatia ajira watu zaidi ya mia moja (100); amb
ao watatokana na waajiriwa wa ndani na wale wa nje (wamashirika hayo ya ndege).

Uwanja huo utakuwa na uwezo wa kupokea idadi kubwa ya ndege kwa wakati mmoja kama
Ifuatavyo;

: ndege tano (5) aina ya Boeing (737-800)

: ndege tatu (3) aina ya Airbus (A.380)

: ndege tatu (3) aina ya Boeing (737-800) pamoja na ndege aina ya Airbus (A.380) na

: ndege mbili (2) aina ya Airbus (A.380) pamoja na ndege moja (1) aina ya Boeing (737-800)

## MAWASILIANO:

Halmashauri ya manispaa Dodoma ina huduma ya mtandao wa mawasiliano ya simu inayotolewa na shirika la simu Tanzania TTCL (TANZANIA TELECOMMUNICATION COMPANY LIMITED). Pamoja na huduma ya intaneti ambayo huwanufaisha watu binafsi na wale wa maofisini, pia kuna mitandao mingine ya simu inayotoa huduma kama hizo ambayo ni: Tigo, Vodacom, Airtel, Zantel na internet café, pia kuna huduma ya posta.

## HUDUMA ZA KIFEDHA:

Kuna benki sita (6) ambazo hutoa huduma za kifedha katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma nazo ni NMB (National Microfinance Bank), CRDB (Coperative and Rural Development Bank), NBC (National Bank of Commerce), Barclays Bank, DTB (Diamond Trust Bank) na Postal Bank. Pia kuna huduma ya ATM kwa saa 24 na kadi za VISA hutumika.

## HUDUMA YA UMEME:

Halmashauri ya Manispaa hupata umeme wake kutoka Gridi ya Taifa na chanzo chake kikubwa ni bwawa la Mtera ambalo huipatia Mji wa Dodoma Megawatt 100 lakini umeme unaotumika ni Megawatt 16.62. Hivyo umeme unaotumiwa ni mdogo ukilinganisha na umeme uliopo, utumiaji huo mdogo unatokana na Mji wetu kutokuwa na shughuli nyingi za viwanda. Na umeme huo wa megawatt 16.62 ni kwa matumizi ya nyumbani na viwanda vidogo vidogo ambavyo havitumii umeme mkubwa, kwa hivyo kuna umeme wakutosheleza kwa wawekezaji wanao taka kuwekeza mjini Dodoma.

## HUDUMA YA MAJI SAFI NA UONDOSHAJI MAJI TAKA:

Huduma hii ya maji safi katika Halmashauri ya manispaa hutokea kwenye chanzo pekee cha uzalishaji maji ambacho ni bonde la Makutopora ambalo lipo nje kidogo ya mji lina jumla ya visima vya uzalishaji maji 22, na 5 ni vyakuchunguza mwenendo wa maji ardhini (observation

boreholes) visima hivi vinauwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo zipatazo 44,000m³ kwa siku lakini kwa sasa vinazalisha mita zaujazo 34,000m³ kwa siku na mahitaji ya maji kwa siku ni wastani wa mita za ujazo 54,000m³ na upatikanaji 45,000m³ kwa sasa. Na kwa upande wa uondoshaji maji taka Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka mjini Dodoma (DUWASA) umeweka mtandao wa uondoshaji majitaka unao jumuisha mabomba makubwa ya kusafirishia maji hayo (trunk sewer) yenye kipenyo cha mm100 na urefu wa km 24.3. Mtandao huu wa kusafirishia majitaka umesanifiwa kuhudumia watu wapatao 423,000 idadi ambayo imekadiriwa kuwa kubwa kuliko idadi ya wakazi wa Manispaa ya Dodoma kwa sasa. Mpaka sasa inawateja wa majitaka wapatao 4.137 hadi Agosti 2010.

Mfumo uliopo wa kutibu majitaka ni mabwawa (waste stabilization ponds-wsps) manne (4) yaliyopo kilometa zipatazo sita (6) toka mjini eneo la Swaswa.Kila bwawa moja lina ukubwa wa mita 400×200×4. Kwa sasa wanampango wa kujenga mabwawa mengine mapya makubwa nane (8) katika eneo la Nzuguni yenye ukubwa wa 400m×400m×8 ambayo yataenda sambamba na ulazaji wa bomba la majitaka lenye kipenyo cha mm1000 na urefu wa km 5.0 ilikukabiliana na ongezeko la wakazi na kupanuka kwa Manispaa yetu.

Kutokana na mahitaji ya maji mjini Dodoma na kuongezeka kwa kasi kubwa kufuatia kukua kwa mji uwekezaji mkubwa unahitajika katika maeneo hayo katika

kipindi kifupi ili ukuaji wa mji uendane na upatikanaji wa huduma hizo, hivyo Duwasa na serikali ipo katika kutafuta fedha za uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika Manispaa.

## UCHUMI KATIKA MANISPAA:

Asilimia 75 ya wakazi wa Dodoma wanajihusisha na kilimo na ufugaji (animal husbandry) na asilimia 25 iliyobaki hujihusisha na biashara (maduka), useremala na vyakula. Shughuli nyingine ni viwanda vidogo na vya kati, ushauri, kazi za ujenzi na shughuli nyingine. Bidhaa kuu zipatikanazo kutoka katika viwanda vilivyopo hapa Dodoma ni mvinyo, magodoro na maji yaliyo fungwa (packed water). Kwenye misitu kuna asali, nta na mbao.

## UWEKEZAJI:-

### ENEO LA KILIMO

Kilimo ni sekta moja wapo ya uwekezaji katika Halmashauri ya manispaa ya Dodoma, hususani katika zao kuu la biashara ambalo ni Zabibu. Uwekezaji wa kiwanda cha mvinyo CETAWICO kumeleta ukombozi kwa wakulima wa zao hili la zabibu, kwani lilishaanza kufa kutokana na kutokuwa na soko la kuaminika. Kiwanda hiki cha mvinyo kilianza na wakulima 50 wa zabibu mwaka 2005 ambao mazao yao yalikuwa yanaipatia lita 80,000 ya juisi ya zabibu (mvinyo), lakini kutokana na mwekezaji huyu kuwa karibu na wakulima na kuwahamasisha (bei zao nzuri) wakulima waliona umuhimu wa kulifufua zao hili

hivyo kupelekea ongezeko la wakulima na kufikia 340 mwaka 2009 ambao hukipatia kiwanda tani 450 za zabibu kwa msimu sawa na lita 1,450,000.





*Kiwanda cha mvinyo CETAWICO na tanki za kuhifadhia mvinyo*



*Zabibu nyeupe*



*Aina za mvinyo ambazo hupatika kiwandani hapo*

## BWAWA LA HOMBOLO

Bwawa la Hombolo ni Bwawa ambalo lipo nje kidogo ya Manispaa km 43 katika kijiji cha Hombolo Bwawani. Bwawa hili lilichimbwa 1957 na Serikali ya Wingereza kwa dhumuni ya mwananchi kutumia Bwawa hili kwa kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya nyumbani, manywesheo ya mifugo na pia kuwapatia kipato na lishe (samaki). Bwawa hili pamoja na madhumuni yake haya mazuri kina chake kinazidi kupungua mwaka hadi mwaka hivyo inahitajika uwondoshaji wa tope ndani ya Bwawa ili kina chake kiongezeke na uhifadhi wa maji uwe mkubwa na kuwezesha wakulima wadogo wadogo kuongeza mashamba yao ikiwa pamoja na kuruhusu/ kuvutia wawekezaji kwani eneo ni kubwa na linafaa kwa kilimo cha aina zote.



*Bwawa la Hombolo*

Eneo lingine la uwekezaji katika sekta ya kilimo na ufugaji. Eneo hili linawapatia faida kubwa sana wawekezaji walioamua kuwekeza katika kilimo cha matunda na mboga mboga pamoja na kuwapatia wawekezaji wenyewe kipato, kilimo hiki kimewapatia wananchi ajira kwa kufanya kazi katika maeneo hayo. Mojawapo ya uwekeazaji huo ni kilimo cha matunda aina ya miembe. Ndugu Willy Mwangason ni mwekezaji katika sekta ya kilimo cha matunda na ufugaji. Ni mwanachama namba 90 katika chama cha wakulima wa maembe Tanzania (AMAGRO), akiwa na shamba lenye ukubwa wa hekta 20 katika eneo la Zuzu umbali wa kilomita 5 kutoka Dodoma mjini, amepanda shambani mwake aina 7 za miti ya miembe ambazo ni Apple, kanti, keti, ngoe, tomi,

satistasion na Alphonso. Aina hizi za miembe zimestawi sana kwa kuwa ardhi ya Dodoma ni nzuri na maji hayako mbali ardhini na pia hali ya hewa ya joto kwani miembe huhitaji joto. Aina hizi za miembe zinazaa sana kuliko miembe ya kienyeji. Na miche ya miembe hii hupatikana chuo cha kilimo SUA Morogoro. Ana miti ya miembe zaidi ya 500 na pia miti ya michungwa. Kwa kuonyesha zao la embe linastawi vizuri mjini Dodoma katika mashindano ya siku ya kuonja embe Duniani yaliyofanjika mwaka 2009 mjini Dar es Salaam embe lililoshinda kwa ubora lilitoka Dodoma mjini kwa mwekezaji huyu. Lilikuwa na uzito wa kilo 2. Kwa kufahamu faida ya kuwekeza katika kilimo ameandaa shamba lenye ukubwa wa hekta 30 kwa ajili ya kupanda mikorosho ambayo nayo hustawi na kuzaa sana. Kauli mbiu ya mwekezaji huyu ni:

**Upatikanaji wa maji kwanza, uwezeshwaji wa wataalamu wa kilimo vyombo vya usafiri na wataalamu hao wapewe elimu ya mara kwa mara iliwaweze kukabiliana na uibukaji wa magonjwa mbalimbali ya mimea.**





*Maembe bora  ambalo hufikia uzito wa kilo mbili*

# MACHINJIO YA DODOMA

Moja ya miradi iliyo wekezwa kwenye manispaa ya Dodoma ni ujenzi wa Machinjio ya kisasa kabisa. Machinjio haya yalijengwa na Serikali kuu kwa kutambua umuhimu wa mji huu, kwa kuwa una mifugo mingi na pia ni njia kuu ya mifugo kutoka mikoa mingine kanda ya kati na kanda ya ziwa. Na upatikanaji wa machinjio yanayo kidhi kanuni za afya ya binadamu. Ujenzi wa machinjio haya yaliigharimu Serikali kuu Shilingi Bilioni 1.926 kupitia wizara husika ya kipindi hicho. Ujenzi huu ulifanyika kwa mfumo wa usanifu, ukiambatana na ufungaji wa mitambo ya kisasa (turnkey contract). Ujenzi ulifanyika 2002 na kumalizika 2004. Uzalishaji ulianza rasmi machi 2005, ilikuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 200 na mbuzi/kondoo 200 kwa siku. Huduma ya uchinjaji hutolewa kwa wafanya biashara wa nyama Manispaa ya Dodoma, na kwa wafanya biashara wa nyama wanaopeleka nje ya mkoa wa Dodoma na nchi za nje kama Kuwait, Oman, Falme za Kiarabu na Jamuhuri ya Demokrasia ya Watu wa Congo (DRC) kwa sasa machinjio haya yamebinafsishwa kwa mwekezaji kampuni ya nyama Tanzania (Tanzania Meet Company, TMC). Nia na madhumuni ni kuwezesha uzalishaji endelevu na wenye tija.

Kuanzia Januari 2010 kampuni ilianza kuzalisha nyama yake yenyewe kwa lengo la kuongezea thamani kabla ya kuiuza ilikuongeza vyanzo vya mapato ya machinjio. Kwanzia machinjio yalipoanza kazi rasmi 2005 mpaka 2009, machinjio yamezalisha idadi ya ng'ombe 116,015,

mbuzi na kondoo 3,053 kwa soko la ndani na lile la nje, idadi ya kondoo 21,134 wenye uzito wa kilogramu 195,318, mbuzi 22,934 wenye uzito wa kilogrmu 198,938 na nyama ya ng‘ombe yenye uzito wa kilogramu 17,940.

Machinjio haya ya kimataifa kwa upande moja yameweza kuipatia serikali fedha za kigeni kutokana na nyama zinazouzwa nje ya nchi, pia watu kutoka eneo la manispaa na wale wa nje ya manispaa wameweza kupata ajira katika machinjio hayo.

Wawekezaji wa ndani na wale wa nje mnakaribishwa kuwekeza katika Halmashauri ya manispaa ya Dodoma kwenye maeneo yaliyoainishwa katika jarida hili.

Tunawakaribisha wawekezaji wote wa ndani nawa nje wanaopenda kuwekeza katika Halmashauri yetu ya Manispaa na kwa Mkoa wetu wa Dodoma kwa ujumla kuwekeza.kwa mawasiliano:

Mkurugenzi:
Halmashauri Ya Manispaa,
S.L.P, 1249, Dodoma.
Simu:2324817
Faksi:23248117/2321550
Email:dodomamunicipality@yahoo.co.uk

Mkurugenzi mkuu CDA
S.L.P, 13, Dodoma.
Simu:+255 26 2324053/2321569
Faksi:+255 26 2323248/2322650
Tovuti:www.cda.go.tz
Barua pepe:info@cda.go.tz

Ofisi ya mkurugenzi mtendaji
DUWASA
Barabara ya chimwaga
S.LP,431, Dodoma.
Simu:+255 2324245/2321179
Faksi:+255 026 2320060
Email:duwasatz@yahoo.com

TANESCO
S.L.P,49, Dodoma.
Simu:+255 26 2322095
Faksi:+255 26 232163
Email:
rm.dodoma@tanesco.co.tz